# *Maneno ya Mungu*

Words of God in Kiswahili

# MANENO
# YA
# MUNGU

***MANENO YA MUNGU***

*Worde of Gods in Swahili*

*Kijitabu hiki kimetafsiriwa na Kamati ya Kitaifa ya Tafsiri ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*

*Na kuchapishwa na Kamati ya Vitabu, Uchapishaji na Usambazaji*

*ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*

*S.L.P. 585, Makongo Juu, Dar es Salaam, Tanzania.*

*Simu: +255-685 637 422*

*Barua Pepe: secretariat@bahai.or.tz.*

*literature@bahai.or.tz*

*Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili na:*

*Kamati ya Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili ya Kitaifa ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*

*Toleo la: 2020*

© Baraza la *Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*

## SALA FUPI YA FARADHI

Nashuhudia, Ewe Mungu Wangu, kwamba Wewe Umeniumba mimi, kukujua wewe na kukuabudu Wewe. Nashuhudia katika wakati huu, juu ya unyonge wangu na uwezo Wako, juu ya umasikini wangu na utajiri Wako.Hakuna Mungu mwingine ila Wewe msaada katika Mashaka, Aliyepo Mwenyewe.

-Baha'u'llah

***(Baha'u'llah alifunua sala tatu za faradhi, ambazo mojawapo inaweza kuchaguliwa na kila muumini na kuisoma kufuatana na maelekezo maalum kwa kila sala.Agizo linalohusiana na sala iliyotolewa hapo juu, ambayo ndiyo fupi kabisa kati ya tatu ni kwamba, ni lazima isemwe mara moja kwa -siku kati ya adhuhuri na machweo.)***

## ALFAJIRI

Mungu wangu na Bwana wangu, Mimi ni mtumishi Wako na mwana wa Mtumishi Wako. Nimeamka kutoka kitandani mwangu katika alfajiri hii wakati Nyota ya Mchana ya umoja Wako imechomoza kutoka Mapambazuko ya amri Yako, na imetawanya wangavu wake juu ya ulimwengu mzima, kulingana na kile kilichoamriwa katika vitabu vya Amri Yako.

Sifa iwe Kwako, Ee Mungu wangu, kwamba tumeamkia kwenye utukufu wa mwangaza wa elimu Yako. Tutelemshie utukufu wa mwangaza wa elimu Yako. Tutelemshie, basi juu yetu, Ee Bwana wangu, kile kitakachotuwezesha kuwa huru na yeyote ila Wewe, na kitatuondolea upendo wote kwa chochote isipokuwa Wewe Mwenyewe. Niandikie, basi, kwa ajili yangu na kwa ajili ya wale ambao ni wapenzi kwangu, na kwa ajili ya ndugu zangu, mke kwa mume kadhalika, mema ya ulimwengu huu na ulimwengu ujao. Tuweke salama, basi , kwa ulinzi Wako usioshindwa, Ewe Mpendwa wa muumbo mzima na Haja ya ulimwengu wote, kutoka wao ambao umewafanya

kuwa udhihirisho wa Yule Mnong’onezi Muovu, ambaye hunong’ona katika vifua vya watu. U Mwenye nguvu kufanya ridhaa Yako. Wewe hakika u Mweza yote , Msaada Mashakani, Aishiye – Mwenyewe.

Mbariki ,Ee Bwana Mungu wangu, Yeye Ambaye Umemuweka juu ya majina Yako bora kabisa, na kwa kupitia Yeye Umetenganisha kati ya wachaji Mungu na waovu, na tusaidie kwa rehema kufanya yale Uyapendayo na utakayo. Wabariki, zaidi ya hao, Ee Mungu wangu, wao Ambao ni Maneno Yako na Herufi Zako, na wao ambao wameelekeza nyuso zao Kwako, na kuugeukia uso Wako, Kusikiliza Mwito wako.Wewe, Kwa kweli, U Bwana na Mfalme wa watu wote, na u Mwenye nguvu juu ya vtu vyote.

-Baha’u’llah

## ASUBUHI

Nimeamka katika himaya Yako, Ee Mungu wangu, na imembidi Yule ambaye anatafuta himaya hiyo adumu ndani ya kimbilio la hifadhi Yako na Ngome ya Kinga Yako. Angaza moyo wangu, Ee Bwana wangu kwa utukufu wa Mapambazuko ya Ufunuo Wako kama ulivyoangaza mwili wangu kwa mwangaza wa asubuhi wa fadhila Yako.

-Baha'u'llah

Nimeamka asubuhi hii kwa rehema Yako, Ee Mungu wangu, na nimeacha maskani yangu nikikutumaini kabisa Wewe, na nikijiweka mwenyewe katika ulinzi Wako. Nitelemshie, basi, juu yangu, kutoka mbingu ya rehema Yako, Baraka kutoka upande Wako na niwezeshe kurudi kwenye maskani yangu kwa usalama kama vile Ulivyoniwezesha kuondoka chini ya ulinzi Wako nikiwa na fikra zangu zimekaziwa kwa uthabiti juu Yako. Hakuna Mungu mwingine ila Wewe, Yule Mmoja, Asiye kifani, Ajuaye yote, Mwenye hekima zote.

-Baha'u'llah

## JIONI

Ee Mungu wangu, Bwana wangu, Lengo la shauku yangu, Mtumishi wako huyu, atazamia kusinzia katika kivuli cha rehema Yako na kupumzika chini ya chandarua ya rehema Yako, akiomba uangalizi Wako na ulinzi wako. Ninakuomba, Ee Bwana wangu, kwa jicho Lako ambalo halisinzii, kuyalinda macho yangu yasitazame mwingine kando Yako. Imarisha, basi kuona kwake ili yaweze kutambua ishara Zako, na kutazama Upeo wa ufunuo wako. Wewe ndiye Yule ambaye mbele ya ufunuo wa uenzi Wake Kipeo cha nguvu kimetetemeka. Hakuna Mungu mwingine ila Wewe, Mwenye enzi, Mtiisha kabisa, Asiyeshurutishwa.

-Baha'u'llah

## MFUNGO

Sifa iwe Kwako, Ee Bwana Mungu Wangu, Nakusihi wewe kwa ufunuo huu ambao kwao giza limegeuzwa kuwa mwanga, ambao kwao Hekalu Lifikiwalo mara kwa mara limejengwa, na Waraka uliokwisha andikwa umefunuliwa, na Gombo Iliyotandazwa imefichuliwa, unitelemshie mimi na hao ambao ni wenzi wangu kile ambacho itackhotuwezesha kupaa angani katika mbingu za utukufu wako mkuu mno, na kututukasa kutokana na doa la mashaka kama yale ambayo yamewazuia wale wenye wasiwasi wasiingie ndani ya hema takatifu la umoja Wako. Mimi ni Yule, Ee Bwana wangu, ambaye amekamata, kwa dhati ugwe wa wema wa upendo Wako, na ameng'ang'ania pindo la rehema Yako na fadhili Zako. Amuru kwa ajili yangu na kwa ajili ya wapendwa wangu mema ya ulimwengu huu na ya ulimwengu ujao. Wape basi, Karama Iliyofichwa ambayo uliamuru kwa wale ambao ni wateule kabisa kati ya viumbe Wako. Hizi ni siku, Ee Bwana wangu, ambazo kwazo Umewaamuru watumishi Wako kuadhimisha mfungo. Amebarikiwa huyo ambaye aadhimisha mfungo kabisa kwa ajili Yako na akiwa amejitenga

kabisa navitu vyote sisipokuwa Wewe tu. Nisaidie mimi na wasaidie wao, Ee Bwana wangu, kukutii Wewe na kufuata maagizo Yako. Wewe kwa kweli, una nguvu kufanya lolote uchagualo. Hakuna Mungu isipokuwa Wewe, Ajuaye Yote, Mwenye Hekima kabisa. Sifa zote ziwe kwa Mungu Bwana wa malimwengu yote.

-Baha'u'llah

## NDOA

Utukufu uwe Kwako, Ee Mungu wangu. Hakika mtumishi Wako huyu na kijakazi Wako Huyu wamejikusanya chini ya kuvuli cha rehema Yako na wameunganika kwa fadhili na ukarimu Wako. Ee Bwana, wasaidie katika dunia Yako hii na Ufalme Wako na uwachagulie kila jema kupitia Baraka Yako na rehema. Ee Bwana, Wathibitishe katika utumishi Wako na uwasaidie katika huduma Yako. Waache wawe ishara za jina Lako ulimwenguni Mwako na uwalinde kupitia vipaji Vyako visivyo kwisha katika ulimwengu huu na ulimwengu ujao. Ee Bwana wameinamia mbele ya ufalme wa neema Yako wakiomba mbele ya milki ya umoja Wako. Hakika wameoana katika utii kwa amri Yako. Wafanye wawe ishara za upatano na umoja mpaka mwisho. Hakika Wewe ni Mwenyezi, Aliyeko kote, na Mwenye enzi.

-Abdu'l-Baha

## KUPONYA

Jina lako ndilo kuponywa kwangu, Ee Mungu wangu, na kukukumuka Wewe ni dawa yangu. Kuwa karibu na Wewe ndio tumaini langu na upendo kwako ndio mwezi wangu. Huruma Yako Kwangu ni kiponyesho changu na msaada kwangu katika ulimwengu huu na ulimwengu ujao. Wewe, hakika ni mwenye Baraka Zote, Ajuaaye yote, Mwenye Hekima zote

-Baha'u'llah

## BARAZA LA KIROHO

*Wakati wowote muingiapo chumba cha mkutano semeni sala hii kwa moyo upumao na mapenzi ya Mungu na ulimi uliotakasika, kutokana na vyote ila kumbukumbu Yake ili kwamba Mwenye uwezo wote aweze kwa neema kuwasaidia kupata ushindi mkuu:*

Ee Mungu, Mungu Wangu! Sisi tu watumishi Wako ambao wameugeukia kwa moyo wa ibada kwenye uso Wako Mtakatifu, ambao tutmejitenga wenyewe kutokana na vyote kando Yako katika Siku hii tukufu. Tumekusanyika katika Baraza hili la Kiroho, tukiunganika katika maoni na Mawazo yetu, tukiwa na madhumuni yetu yamepatanishwa kutukuza Neno lako kati ya wanadamu. Ee Bwana, Mungu wetu! Tufanye ishara za uongozi Wako mtakatifu, bendera za Imani yako iliyotukuka kati ya watu, watumishi kwenye Ahadi Yako Kuu, Ewe Bwana wetu Uliye Juu kabisa, Wadhihirishaji wa umoja wako Mtakatifu katika ufalme Wako wa Abha, na nyota za kung'aa ziwakazo juu ya sehemu zote. Bwana! Tusaidie kuwa bahari zisukasukazo kwa mawimbi ya neema Yako ya ajabu, mito itiririkayo kutoka

Vilele Vyako vilivyotukuka kabisa, matunda memema juu ya mti wa Imani Yako ya mbinguni, miti ipepeayo kwa pepo za Baraka yako katika shamba Lako la mizabibu la mbinguni. Ee Mungu! Zifanye roho zetu zitegemee aya za umoja Wako mtakatifu, mioyo yetu ikichangamshwa na mmiminiko wa neema Yako, ili tuweze kuunganika kama vile mawimbi ya bahari moja na kuunganishwa pamoja kama miale ya nuru Yako ing'aayo; ili mawazo yetu maoni yetu, hisia zetu, viweze kuwa kama uhalisia mmoja vikidhihirisha moyo wa umoja ulimwenguni kote. Wewe ni Mwenye Neema, Mjalia, Mpaji, Mwenyezi, Mwenye rehema, Mwenye huruma.

-Abdul-Baha

## SALA KWA WATOTO NA VIJANA

Ee Mungu! Mlee mtoto huyu mchanga katika kifua cha upendo wako, na umpe maziwa kutoka kutoka kifua cha majaliwa yako. Palilia mche huu mchanga katika bustani ya waridi ya upendo Wako na umsaidie kukua kupitia manyunyu ya Baraka Yako. Mfanye mtoto wa Ufalme na umwongoze kwenye milki Yako ya mbinguni. Wewe u Mwenye nguvu na mwema na Wewe U Mpaji, Mkarimu, Bwana wa baraka zisizo kifani.

-Abdu'l- Baha

Ee Mungu! Waelimishe watoto hawa. Watoto hawa ni miche ya kiunga Chako cha miti ya matunda, maua ya konde Lako, mawaridi ya bustani yako, acha mvua yako iwanyeshee, Jua la ukweli liwaangazie kwa upendo Wako. Acha upepo Wako mwanana uwaburudishe ili Kwamba wafunzwe, wakue na kuendelea na waonekane katika uzuri wa juu kabisa. Wewe u Mpaji! Wewe U Mwenye huruma.

-Abdu'l-Baha

Ee Bwana! Mfanye kijana huyu mwangavu na ujalie Baraka Yako juu ya kiumbe huyu masikini. Umjalie maarifa na umpe nguvu zaidi kwenye kila mapambazuko na umkinge katika kivuli cha ulinzi Wako ili aweze kuondolewa katika makosa, aweze kujitoa kwa moyo wa Ibada katika huduma ya Hoja Yako, aweze kuwaelekeza wapotovu, kuwaongoza wadhilifu, kuwaweka huru mateka na kuamsha wazembe ili wote waweze kubarikiwa kwa kumbukumbu na sifa Yako. Wewe ndiye mwenye uwezo na mwenye nguvu.

-Abdu'l-Baha

Ee Mungu, niongoze, nilinde, nifanye taa ing'aayo na nyota angavu. Wewe ni Mwenye uwezo na Mwenye nguvu.

-Abdu'l-Baha

## MCHANGO KWENYE AKIBA

*Marafiki wote wa Mungu.... Wanapaswa wachangie kwa kiasi kiwezekanacho, hata kama sadaka yao ndogo jinsi gani. Mungu haitwishi roho msingo zaidi ya uwezo wake. Michango kama hiyo ni lazima ije Kutoka kwenye vituo vyote na ktoka waumini wote... Enyi marafiki wa Mungu! Muwe na hakika kuwa kutokana na michango hii, kilimo chenu,viwanda vyenu,na biashara zenu vitabarikiwa kwa nyogeza za namna nyingi,kwa vipaji vyema na majaliwa.Yeye ajalia na tendo moja jema atapokea tunzo ya mara kumi.Hakuna shaka kwamba Bwana aishiye atawathibitisha kwa wingi wote watumiao utajiri wao katika njia Yake..*

Ee Mungu. Mungu wangu! Ng'arisha paji za nyuso za wapenzi Wako wa kweli, na uwasaidiei kwa majeshi ya kimalaika wa ushindi wa uhakika. Imarisha miguu yao kwenye njia Yako iliyonyooka, na kutoka kwenye Baraka yako ya kale fungua mbele yao milango ya neema Zako; Kwani wanatumia katika njia yako kile ulichowalia wakilinda Imani Yako, wakiweka imani yao katika

kukukumbuka wewe, wakitoa mioyo yao kwa ajili ya upendo Wako, na bila kuzuia walicho nacho katika kusujudua Uzuri Wako na katika kutafuta njia za kukupendeza wewe. Ee Bwana wangu! Amuru kwa ajili yao fungu tele, fidia iliyokusudiwa na tunzo la hakika. Hakika wewe ndiye Mhifadhi , Msaidizi, Mkarimu, Mwenye Baraka, Mpaji daima.

Abdu’l-Baha

## SALA KWA AJILI YA MAREHEMU

Sala hii ndefu ya Faradhi kwa ajili ya marehemu itumike kwa Wabahai wenye umri wa miaka kumi na tano na zaidi.'Ndiyo sala pekee ya Faradhi ya Kibaha'i ambayo hughaniwa katika mkusanyiko ; ni ya kusemwa na muumini mmoja wakati wote waliopo wakiwa wamesimama. Hakuna masharti kuelekea Kibla wakati wa kusema sala hii."

Ee Mungu Wangu! Huyu ni mtumishi Wako na mwana wa mtumishi Wako ambaye amekuamini Wewe na ishara Zako, na kuelekeza uso wake kwako, amejitenga kabisa kutoka kwa yvote ila Wewe. Wewe hakika, Ndiwe wa wale ambao huonyesha reheme, mwenye rehema kabisa. Mtendee, Ee Ewe Ambaye husamehe dhambi za watu na kusetiri kasoro zao, kama istahilivyo mbingu ya Baraka Yako na bahari ya rehema Yako. Mjalie kuingia ndani ya mipaka ya rehema Yako bora kabisa ambayo ilikuwepo kabla ya kuanzishwa kwa dunia na mbingu. Hakuna Mungu ila Wewe, msamehevu- daima, Mkarimu kabisa.

*Ndipo tena, arudie mara sita maamkizi "Allah'u'abha" na tena arudie mara kumi na tisa kila aya zifuatazo:*

Sote, hakika, twamuabudu Mungu x19
Sote, hakika ,twasujudu mbele ya Mungu x19
Sote, hakika, tumejitoa kwa Mungu x19
Sote, hakika ,twamsifu Mungu x19
Sote, hakika, twatoa shukrani kwa Mungu x19
Sote, hakika, tuwenye subira kwa Mungu. x19

(*ikiwa marehemu ni mwanamke, hebu aseme: huyu ni mtumishi Wako wa kike na binti wa mtumishi Wako wa kike n.k...)*

-Baha'u'llah

Ee Mungu wangu! Ee Ewe msamehe dhambi, mtoaji thawabu, mwondoa huzuni! Hakika, nakusihi kusamehe dhambi za wale walioacha vazi la kimwili na wamepaa kwenye ulimwengu wa kiroho. Ee Bwana wangu! Uwatakase kutokana na makosa, ondoa huzuni zao, na ubadilishe giza lao katika mwanga. Wafanye waingie bustani ya furaha, uwatakase kwa maji safi kabisa, na uwajalie waone utukufu Wako kwenye mlima ulio bora kabisa.

-Abdu'l-Baha

## SALA ZA UMOJA

Utukufu uwe Kwako Ee Mungu, kwa ajili ya Ufunuo wa Pendo lako kwa wanadamu! Ee Ewe uliye Uzima na Mwanga wetu, ongoza watumishi Wako katika njia Yako, ututajirishe ndani Yako na kuwa huru kwa yote ila Wewe tu. Ee Mungu, utufundishe umoja Wako na utupe utambuzi wa Umoja Wako ili tusione yeyote ila Wewe. Wewe U Mwenye rehema na Mpaji wa ukarimu! Ee Mungu, washa moto wa upendo Wako katika mioyo ya wapendwa Wako ili uteketeze mawazo ya kila kitu ila Wewe. Tufunulie, Ee Mungu milele Yako iliyotukuka kwamba Wewe umekuwako na utakuwako, na kwamba hakuna Mungu mwingine ila Wewe tu. Hakika faraja na nguvu vinapatikana Kwako.

-Baha'u'llah

Ee Mungu wangu! Ee Mungu wangu! Unganisha mioyo ya watumishi Wako na uwafunulie kusudi Lako lililo kuu. Wafuate amri Zako na kukaa katika sheria Yako. Uwasaidie, Ee Mungu katika jitihada yao, na uwape nguvu kukutumikia Wewe. Ee Mungu usiwaache peke

yao bali uongoze hatua zao kwa nuru ya maarifa Yako na ufurahishe roho zao kwa upendo Wako. Hakika, wewe ndiye Msaidizi na Bwana wao.

-Baha'u'llah

Sema: Ee Mungu, Mungu wangu! Vika kichwa changu kwa taji la haki na paji la uso wangu kwa pambo la uadilifu, Wewe hakika U Mwenye vipaji na baraka zote.

-Baha'u'llah

Ee Mungu wangu! Nakuomba kwa Jina Lako tukufu kabisa, Kunisaidia katika lile litakalofanya shughuli za watumishi Wako kufanikiwa, na miji Yako kustawi. Wewe kweli una nguvu juu ya vitu vyote.

-Baha'u'llah

Mungu jalia kwamba nuru ya umoja iweze kufunika dunia yote, na kwamba mhuri "Ufalme ni wa Mungu" uweze kupigwa juu ya paji la uso la watu wake wote.

-Baha'u'llah

Kuna mwondoa shida yeyote isipokuwa Mungu? Sema: Mungu asifiwe! Yeye ni Mungu! Wote ni watumishi Wake, na wote wanaishi kwa mapenzi Yake.

-Bab

Ee Mungu,changamsha na furahisha roho yangu. Takasa moyo wangu, Ng'arisha fikra zangu. Naweka shughuli zangu zote mkononi Mwako. Wewe ndiwe kiongozi wangu na kimbilio langu. Sitakuwa na majuto wala kuhuzunika tena, Nitafurahi na kuchangamka. Ee Mungu! Sitajawa na mashaka tena, wala sitaacha taabu zinisumbue tena. Sitaishi kwa vitu visivyofaa maishani. Ee Mungu! Wewe ni mwenye huruma zaidi kwangu kuliko ninavyo jihurumia mwenyewe. Najitoa mwenyewe kwako Ee Bwana.

-Abdu'l-Baha

Ee Bwana Wangu, Mpendwa wangu. Haja yangu! Nifanye rafiki katika ukiwa wangu na ufuatane nami katika uhamisho wangu. Ondoa huzuni yangu, Nifanye kujitoa kwa moyo wa ibada kwa Uzuri Wako. Niondoe kwa vyote isipokuwa

wewe. Nivutie kupitia manukato Yako ya utakatifu. Nifanye kuwa mshiriki katika Ufalme Wako na wale ambao wamejitenga na vyote isipokuwa Wewe, ambao hutamani sana kuhudumia kizingiti Chako kitakatifu na ambao huvumilia kufanya kazi katika Hoja Yako. Uniwezeshe kuwa mmoja wa watumishi Wako wa kike ambao wamepata ridhaa Yako njema. Hakika, Wewe ni mwenye Rehema, Mkarimu.

-Abdu'l-Baha

Ee Bwana Mungu Wangu! Wasaidie wapendwa Wako kuwa imara katika Imani Yako, Kutembea katika njia Zako, kuwa thabiti katika Hoja Yako. Wape neema Yako kuzuia mashambulio ya nafsi na tamaa, kufuata nuru ya Uongozi Mtakatifu. Wewe ni Mwenye nguvu, Mwenye rehema, Aishiye Mwenyewe, Mpaji, Mwenye huruma, Mwenyezi, Mkarimu kabisa.

-Abdu'l-Baha

Bwana , sisi tu watu wa kuhurumiwa, utupe kibali Chako; tu maskini, utupe fungu kutoka wingi wa ukwasi Wako; tu wenye haja ututosheleze; tumetahayarishwa, utupe neema yako. Ndege wa anga na wanyama wa konde wapokea chakula chao kutoka Kwako kila siku na viumbe vyote vina ulinzi na upendo Wako. Usimnyime mnyonge huyu neema Yako ya ajabu na umjalie roho yake dhaifu Baraka kwa uwezo Wako. Utupe chakula chetu cha kila siku na utuongezee maisha yetu, ili tusitegemee yeyote ila Wewe, tuzungumze nawe, tutembee katika njia Zako na kutanganza mafumbo yako. Wewe U Mwenyezi na Apendaye na Mpaji wa wanadamu.

-Abdu'l- Baha

Ee Bwana! Sisi tu wanyonge, tuimarishe, Ee Mungu! Tu wajinga, tufanye wajuzi. Ee Bwana tu maskini, tufanye matajiri. Ee Mungu! Tu wafu, tuhuishe. Ee Bwana! Sisi tu fedheha yenyewe; Ee Bwana tutakuwa kama nyota zimemetekazo. Usipotusaidia, tutakuwa na hali ya chini kuliko udongo. Ee Bwana! Tuimarishe. Ee Mungu! Tujalie ushindi. Ee Bwana! Tuwezeshe

kushinda nafsi na tamaa. Ee Bwana! Tuokoe kutoka katika utumwa wa mambo ya kidunia. Ee bwana! Tuhuishe kupitia pumzi ya Roho Mtakatifu ili tuamke kukutumikia, tujishughulishe katika kukuabudu Wewe na kujibidiisha wenyewe katika ufalme Wako kwa ukweli kabisa. Ee Bwana, U mwenye Rehema.

-Abdu'l-Baha

Ee Mungu, Mungu wangu! Wakinge watumishi Wako waaminifu na maovu ya tamaa Walinde na jicho Lako la upendo katika chuki, karaha na kijicho, uwahifadhi katika Neno Lako lisilopotoka wawe salama kwa mishale ya mashaka, wafaye wajumbe wa ishara Zako tukufu, ng'arisha nyuso zao kwa miale inayong'aa itokayo katika chimbuko la umoja wako mtukufu, furahisha nyoyo zao kwa maneno yatokayo katika ufalme wako mtukufu natia nguvu viuno vyao kwa nguvu itokayo katika milki Yako tukufu. Wewe U Mkarimu, Mlinzi, Mwenyezi na Mwenye rehema.

-Abdu'l-Baha

Ee Mungu! Ewe Mungu! Huyu ni ndege aliyevunjika mabawa yake na kuruka kwake ni shida sana. Msaidie ili kwamba aweze kuruka kwa upeo wa ufanisi na wokovu, wezesha kuruka kwake kuwe kwa shangwe kuu na furaha na katika nafasi isiyo na kikomo, inua sauti yake tamu katika Jina Lako Kuu kabisa ndani ya sehemu zote, changamsha masikio na mwito huu, na ng'arisha macho kwa kutazama dalili za maongozi! Ee Bwana! Mimi ni mpweke, mmoja na aliye chini. Kwangu mimi sina wa kutegemea ila wewe, sina wa kunihifadhi kando Yako. Nithibitishe katika kazi yangu, nisaidie na majeshi ya malaika Wako, nifanye mshindi katika kuendeleza neno Lako na uniwezeshe kunena kutoka kwa hekima Yako juu ya viumbe Vyako. Hakika Wewe U Mtunza masikini na Mtetezi wa walio wadogo na kweli U mwenye nguvu, Mwenye uwezo na Asiyeshurutishwa!

-Abdu'l- Baha

## MATEUZI KUTOKA “MANENO YALIYOFICHWA” YA BAHA’U’LLAH

### EWE MWANA WA KUWA!

Paradiso yako ni upendo Wangu, makao yako ya mbinguni ni muungano tena Nami. Ingia humo na wala usingojee. Hili ndilo lililoamriwa kwa ajili yako katika ufalme Wetu ulio juu na milki Yetu inayotukuka.

### EWE MWANA WA ROHO!

Usiniombe kile tusichopendelea kwa ajili yako, hivyo ridhika na kile tulichoamuru kwa ajili yako, kwa maana hicho ndicho kinachokufaa kama utajiridhisha nacho.

### EWE MWANA WA MTU!

Usinong’one dhambi za wengine iwapo wewe mwenyewe ni mtenda dhambi, Kama ukiivunja amri hii utakuwa umelaaniwa, na kwa jambo hili Mimi nashuhudia.

**EWE MWANA WA MTU!**

Usimnyime mtumishi Wangu anapotaka kitu chochote kutoka kwako, kwa maana uso wake ni uso Wangu; kwa hiyo tahayari mbele Yangu.

**EWE MWANA WA KUWA!**

Jifanyie hesabu mwenyewe kila siku kabla hujaitwa kwenye kutoa hesabu; kwa maana kifo, bila onyo kitakufikia na utaitwa kutoa hesabu ya matendo yako.

**EWE MWANA WA MWENYENZI!**

Nimekifanya kifo kuwa mjube wa kukuletea furaha. Kwa nini basi unasikitika? Niliiumba nuru ili ikuangazie utukufu wake juu yako. Kwa nini unajificha kutoka kwake?

**EWE MWANA WA ROHO**

Kwa habari njema ya nuru nakusalimu; furahia! Kwenye baraza la utakatifu nakuita; udumu humo ili uweze kuishi kwa amani milele.

**EWE MWANA WA MTU!**

Kama neema itakuangukia, usishangilie, na kama udhilifu ukikujia, usisikitike, kwani vyote vitapita na vitakwisha.

**EWE MWANA WA KUWA!**

Kama umasikini utakufikia, usihuzunike moyoni; kwa maana kuna wakati Bwana wa neema atakutembelea. Usiogope udhilifu, kwa maana utukufu siku moja utakaa juu yako.

**EWE MWANA NA KUWA!**

Usijishughulishe na ulimwengu huu kwa maana kwa moto twaipima dhahabu na kwa dhahabu twawapima watumishi Wetu.

**EWE MWANA WA KUWA!**

Moyo wako ni makao Yangu; utakase kwa mshuko Wangu, Roho yako ni mahali pangu pa ufunuo; isafishe kwa ajili ya udhihirisho Wangu.

**EWE RAFIKI!**

Katika bustani ya moyo wako usipande kingine ila miwaridi ya upendo, na kutoka ndege mwimbaji wa upendo na shauku usiachilie mkono wako. Thamini urafiki wa wenye haki na uepukane na ushirikiano wowote na waovu.

## EWE MWANA WA VUMBI!

Yapofushe macho yako ili uweze kuuona uzuri Wangu; ziba masikio yako ili usikie sauti Yangu nyororo; imwage elimu yote ili utwae sehemu ya elimu Yangu; na jitakase kutoka utajiri ili upate sehemu ya kudumu kutoka bahari ya utajiri Wangu wa milele. Pofua macho yako, yaani kwa vitu vingine vyote isipokuwa uzuri Wangu; ziba masikio yako kwa vyote isipokuwa neno Langu; imwage elimu yote isipokuwa elimu Yangu; ili kwa macho safi, moyo safi na sikio la makini uweze kuingia baraza la utakatifu Wangu.

## EWE UMBILE LA VUMBI LIENDALO!

Natamani mazungumzo nawe lakini wewe huweki tumaini Kwangu. Upanga wa uasi wako umeuangusha mti wa tumaini lako. Kila wakati niko karibu nawe lakini wewe daima uko mbali Nami. Nimekuchagulia utukufu wa milele, Lakini wewe umejichagulia aibu isiyo na mpaka. Rudi muda ungalipo bado na usipoteze nafasi yako.

**EWE MWANA WA DUNIA!**

Kama ungelikuwa na Mimi; usimtafute yeyote zaidi Yangu; na kama ungeutazama uzuri Wangu fumba macho yako kwa dunia na yote yaliyomo ndani yake; kwa maana mapenzi Yangu na mapenzi ya mwingine zaidi Yangu, kama moto na maji haviwezi kukaa pamoja katika moyo mmoja.

**EWE MGENI ULIYEFANYWA RAFIKI!**

Mshumaa wa moyo wako huwashwa kwa mkono wa uwezo Wangu, usiuzime kwa pepo za upinzani na nafsi na shauku. Mponyaji wa maradhi yako yote ni kunikumbuka Mimi, usisahau jambo hilo. Ufanye upendo Wangu kuwa hazina yako na uutunze kama macho yako yenyewe na uhai.

**ENYI MATAJIRI DUNIANI!**

Maskini kati yenu ni dhamana Yangu; itunzeni dhamana Yangu; na msidhamirie tu kwenye starehe zenu wenyewe.

**EWE MWANA WA SHAUKU!**

Jitakase kutokana na najisi ya utajiri katika amani kamili jongelea milki ya umasikini; ili kutoka katika chemchemi ya kujitenga uweze kunywa mvinyo wa maisha ya milele.

**EWE MWANA WA KIJAKAZI WANGU!**

Kunywa kutoka katika ulimi wa mwenye rehema mkondo wa siri takatifu, na kutazama kutoka katika mapambazuko ya Maneno Matakatifu fahari iliyofunuliwa ya Nyota ya mchana ya hekima. Panda mbegu za hekima Yangu takatifu katika udongo safi wa moyo na uzinyeshee kwa maji ya uhakika, ili maua (ya hyacinth) ya elimu na hekima yaweze kuchipua mabichi na ya kijani kutoka katika mji mtaktifu wa moyo.

## MATEUZI KUTOKA KATIKA BAADHI YA NYARAKA ZA BAHA'U'LLAH

Hakika nasema, hii ndiyo siku ambapo wanadamu waweza kuona uso, na kusikia sauti ya mwahidiwa. Mwito wa Mungu umepaazwa na nuru ya uso Wake imeinuliwa juu ya watu. Yampasa kila mtu kufutilia mbali alama ya kila neno la upuuzi kutoka kwenye ubao wa moyo wake na kutazama kwa akili iliyo wazi na isiyokuwa na upendeleo, juu ya ishara za Ufunuo wake, ushuhuda wa Ujumbe wake na dalili za utukufu Wake.

Enyi watoto wa watu! Kusudi la asili linalotia uzima Imani ya Mungu na Dini Yake ni kulinda shughuli na kukuza umoja wa jamii ya wanadamu, na kuongeza moyo wa upendo na upatano kati ya watu. Msiiruhusu kuwa chanzo cha ufarakano na ugomvi, cha chuki na uadui. Hii ndiyo njia iliyonyooka, msingi uliosimikwa na usiotikisika. Chochote kinacho simamishwa juu ya msingi huu, mabadiliko na nasibu za dunia haviwezi kamwe kudhoofisha nguvu zake, wala mageuzi ya karne zisizohesabika kuharibu umbo lake.

Jizamisheni katika bahari ya maneno Yangu ili muweze kufumbua siri Zake na kugundua vito vyote vya hekima ambavyo vimefichika katika vina vyake. Angalieni msije mkasitasita katika kusudi lenu kuukubali ukweli wa Hoja hii – Hoja ambayo kupitia kwake nguvu zisizodhihirika za uwezo wa Mungu zimedhihirishwa na enzi Yake kusimamishwa. Kwa nyuso zinazong'aa kwa furaha , kimbilieni Kwake. Hii ndiyo Imani ya Mungu isiyobadilika, ya kale na ya milele siku zijazo. Mwache Yule atafutaye aipate, na kwa Yule ambaye amekataa kuitafuta – hakika Mungu ni wa kujitosheleza, juu ya mahitaji ya viumbe wake. Sema: Hii ndiyo mizani yenye hakika ambayo mkono wa Mungu umeishika, ambamo wote walio mbinguni na wote walio duniani wanapimwa, na hatima yao kuamuriwa ikiwa mkono wa wale ambao husaidika na kutambua ukweli huu. Sema: Kwayo masikini wametajirishwa, wenye elimu kuangaziwa, na watafutaji wamewezeshwa kupaa hadi mbele ya Mungu. Angalieni , msiifanye chanzo cha ufarakano kati yenu. Muwe imara kama mlima usiotikisika katika Hoja ya Bwana wenu mwenye nguvu, Apendaye.

Uwe mkarimu katika ufanisi na mwenye shukrani katika taabu. Uwe mwenye kustahili uaminifu wa jirani yako na umwangalie kwa uso mwangavu na wa kirafiki. Uwe hazina kwa masikini, mwonyaji kwa tajiri, mwitikaji kwenye mlio wa mhitaji, mhifadhi wa utakatifu wa ahadi yako. Uwe na haki katika hukumu yako na mwangalifu katika maneno yako. Usiwe mwenye dhuluma kwa mtu yeyote , na uonyeshe upole wote kwa watu wote. Uwe kama taa kwa wale ambao hutemebea katika giza, furaha kwa mwenye huzuni, bahari kwa mwenye kiu, pepo kwa wenye fadhaa, msaidizi na mtetezi wa Yule aliyepatwa na dhuluma. Acha ukamilifu na tabia ya unyofu vitofautishe vitendo vyako vyote. Uwe nyumba kwa mgeni, kitulizo kwa mwenye mateso, tegemeo kuu kwa mkimbia hatari. Uwe macho kwa kipofu, na nuru ya uongozi kwa miguu ya mpotovu. Uwe pambo kwa uso wa ukwel, taji kwa paji la uso la uaminifu, nguzo ya hekalu la haki, pumzi ya uzima kwa mwili wa mwanadamu, safina juu ya bahari ya hekima, jua katika mbingu ya Baraka, kito cha thamani kwenye taji la hekima, nuru ing'aayo katika mbingu ya kizazi chako, tunda juu ya mti wa unyenyekevu.

Uzuri wa Kale amekubali kufungwa kwa minyororo ili kwamba binadamu waweze kufunguliwa kutoka kwenye utumwa wao, na amekubali kufanywa mfungwa ndani ya ngome hii kuu kabisa kwamba dunia yote iweze kufikia kwenye uhuru wa kweli. Amekunywa mashinda ya kikombe cha huzuni, ili watu wote wa dunia waweze kupata shangwe ya kudumu na kujazwa na furaha. Hii ni kwa huruma ya Bwana wenu, Mwenye huruma, Mwenye rehema kabisa. Tumekubali kushushwa, Ee waamini katika Umoja wa Mungu, ili muweze kutuzwa, na tumepatwa na mateso ya namna nyingi, ili muweze kufanikiwa na kustawi. Yeye ambaye amekuja kujenga upya ulimwengu wote, tazama, njisi wao ambao wamejifanyizia washirika na Mungu, wamemlazimisha Yeye kukaa ndani ya miji ya majangwa kabisa!

## KUTOKA KATIKA MAANDIKO YA ‘ABDU’L-BAHA

Ee ewe uliyegeuzia uso wako kuelekea kwa Mungu! Fumba macho yako kwa vitu vyoye vingine, na uyafumbulie kwenye milki ya Mtukufu Kabisa. Omba chochote ukitakacho Kwake pekee; tafuta chochote ukitafutacho kutoka Kwake pekee. Kwa mtazamo mmoja Ajalia taraja mia moja elfu, kwa mtupo wa jicho. Huponyesha magonjwa mia moja elfu yasiyotibika, kwa tazamo la mara moja hutoa kitulizo kwa kila donda, kwa mwinamo wa kichwa huachilia mioyo kutoka kwenye pingu za huzuni. Hufanya Afanyavyo, na tuna kimbilio gani? Hutimiza Nia Yake Huamuru Alitakalo. Hivyo ni bora zaidi kwako kuinamisha kichwa chako katika utii, na uweke tumaini lako katika Bwana Mwenye rehema kabisa.